

KUBANWA NDIYO MSINGI WA MAFANIKIO

Kubanwa ni kuwekwa katikati ya kitu au vitu na kutumiwa nguvu kukusonga pande zote. Mfano wa kitu kilichobanwa ni kufuli na mlango, mtego na mzoga, karatasi na pini, na mambo mengine kadha wa kadha yanayofanana na hayo. Maneno mengine ya lugha ya Kiswahili yenye kukaribiana maana ni; gandamiza, kamata, nasa, au/na fyanda.

Mafanikio ni upatikanaji wa kitu au mahitaji yaliyokuwa yamekusudiwa.

Kubanwa kunakoweza kuwa msingi wa mafanikio ni kama ifuatavyo;

Uchumi wa familia; Wazazi na walezi wengi hutokea wanapata fedha za kukidhi mahitaji ya familia ingawa fedha hizo hazitokani na vyanzo vyenye uhakika. Mfano malipo ya karo za shule ambayo mara nyingi hutolewa kwa muda maalum au fedha za matibabu ambazo zinalazimika zitolewe kwa wakati ili kuokoa maisha. Cha ajabu, mtoto/watoto wakishahitimu masomo na upatikanaji wa fedha unakata. Ingawa watu wengi uhisi wangeweza ‘ku-save’ na kuwa na ziada.

Hali hii inadhihirisha kuwa binadamu wasipobanwa iwe kwa kutumia sheria, kanuni, taratibu za zilizowekwa, mila na desturi, dini, au misingi yoyote ya kimaisha hapa duniani; hawawezi kujisimamia. Mtu atabweteka, atakuwa mvivu, atajiachia na kuanza dharau, ataridhika na kidogo na kuacha mihangaiko, ataanza kudai vitu vya ziada, ataanza kuchukulia poa kila nyongeza! Mwishowe atashindwa kuendelea na kuona anaonewa, ananyanyaswa, anadhulumiwa, anatengwa, analazimishwa, ataiba, visababu visivyokuwa na kichwa wala miguu kwa kufikiria kuna mahali ataishi kusikokuwa na yale aliyoyakwepa.

Matokeo yake mtu huyo ndoa itamshinda, kazi zitamshinda, cheo atanyang'anywa, *atatumbuliwa*, atafeli mitihani, atabaki masikini, maradhi yatamwandama, n.k

Mafanikio binafsi; Mfano kwenye biashara; ili biashara iendeleo lazima kuwe na jambo litalomfanya mmiliki wa biashara kuwa makini kufuatilia biashara yake. Mfano mzuri ni mkopo, upatu, VICOBA, mwanahisa mwenza, vikundi, au wateja wenye ubia na nafasi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa kila siku.

Wabia watahitaji huduma au bidhaa kwa wakati hivyo lazima mfanyabiashara azingatie hilo (kuchimbua ubongo) na kusimamia vizuri tenda ili hasipoteze wateja. Mkopo utambana mmiliki wa biashara kusimamia mapato ili aweze kupata marejesho. Matokeo ya ufuatiliaji huo, mapato yatakua na biashara kukua pia. Kilichofanya ufuatiliaji makini ni mkopo au ubia, bila ya hivyo mfanyabiashara ataweza kuridhika na kile kitakachopatikana. Haijalishi ni kidogo au kikubwa.

Sumu ya utekelezaji; Mapenzi yanalalamikiwa kuwa ni chanzo cha uzembe kazini. Ubongo wa binadamu hauna mapenzi bali una mazoea! Hivyo chanzo sio mapenzi kwa kuwa mapenzi ni matokeo ya mazoea hivyo kugeuka kilainishi cha sheria na taratibu za kazi. Pale pa gumu kama chuma, panaanza kuwa laini kama boflo.

Sheria na taratibu za ofizi/kazi ndizo zinazowafanya watumishi/wafanyakazi/waajiri kuchimbua ubongo na kujikuta wote ni watumwa wa ofisi. Hata kama mwajiri hawezi kuacha kutekeleza majukumu yake kwa sababu mfumo utamlazimisha kufuata taratibu. Mfano kulipa mishahara ya wafanyakazi, bosu atachimbua ubongo ili

apate fedha za kulipa mishahara na stahiki nyingine za wafanyakazi. Kutengeneza bidhaa zenye ubora, kulinda usalama wa wafanyakazi na mali za ofisi n.k. Endapo kusingelikuwa na sheria na taratibu hizo, mabosi wengi wasingejisumbua kuchambua ubongo mwishowe wasingewalipa wafanyakazi wao.

Hivyo kazi nyingi zisingetekelezwa kwa ubora unaotakiwa kwa kukosa watu wenye weledi wanaotokana na ‘experience’ ya kazi. Mapenzi kwenye kazi yanapindisha sheria na taratibu za ofisi zilizowekwa kwa mujibu wa sheria. Kama vile badala ya mfanyakazi kuwepo kazini, atakwenda nyumbani.

Alikadhalika chuki na wivu wa mapenzi, dharau kwa wateja au watumiaji wengine wa ofisi, uongo, uvivu na mwishowe mtendaji/watendaji wakiendelea kutochimbua ubongo; watapoteza sifa za utumishi lakini watalazimika kuwepo kwenye ajira kutokana na ukaribu wa bosu kama uhusiano ni wa bosu na mwajiriwa. Au wafanyakazi wenyewe kwa wenyewe, kutumia muda mwingi kujadili mapenzi badala ya kufanyakazi.

Mwishowe maendeleo yatakosekana kutokana na sheria za ofisi kupuuzwa na wafanyakazi kuanza kupumzika na kujipangia au kujichagulia kipi kifanywe na kipi kiachwe!

Pia nafananisha ubongo wa binadamu wa kawaida na mti (mmea). Kama hautapogolewa kwa kukatwa matawi machanga kwa kutumia kisu kikali, matawi yatarefuka na kuzuia watu kupita. Ubongo utamuongoza mtu kuwa na kiburi kitakachopelekea kutamani afanyiwe jambo badala ya yeye kufanya mwenyewe au kuruhusu watu wafanye kwa moyo mkunjufu.

Wanafunzi kubanwa ili wafaulu masomo yao na hatimae kutoka kimaisha. Mwanafunzi anayeachwa azurure mitaani kama kuku wa kienyeji hawezi kuwa na mafanikio mazuri katika masomo yake. Ikitokea kuwa mwenye akili nyingi basi atasimamishwa au kufutwa shule kwa utovu wa nidhamu.

Kubali ubanwe ili upate maendeleo